

"POSHO NA RUSHWA HAINA TOFAUTI NA KILIO NA KICHEKO"

30 Julai, 2020



Maana za maneno hayo katika lugha ya Kiswahili yapo kwenye kamusi na matini mbalimbali. Mimi nitaelezea mfanano wake.

Kulia na **kucheka**, vyote ni hisia. Mtu analia awapo na huzuni, aibu, maumivu, machungu, au furaha. Alikadhalika na kucheka ni vivyo hivyo.

Posho ni malipo ya ziada anayopewa/ kulipwa mtu ili kukamilisha kazi au huduma kwa haraka. Mara nyingi inakuwa na muda maalum. Hivyo kazi zote zenye posho zinakamilika kwa haraka na vizuri sana kuliko

zisizokuwa na posho, wataalamu wa mambo wametafsiri kuwa ni motisha katika kazi. **Rushwa** nayo kazi yake inafanana na posho yaani ni malipo ya ziada yanayomwezesha mtoa rushwa kufanyiwa kazi yake ngumu kuwa nyepesi / kurahisishwa na kukamilika kwa wakati na uhakika na mpokea rushwa inakuwa ni motisha.

Sasa basi, kila mwenye kazi ya ziada anaandaa malipo kwa watendaji wake ili mambo yaende kama yalivyopangwa kwenye mpangokazi. Iwe ni serikali, taasisi, kampuni au mtu binafsi.

Hivyo tafsiri ya rushwa katika lugha ndiyo hatia na tafsiri ya Posho ndiyo uhalali wake lakini kazi za hayo mambo mawili ni moja au sawa.

Hivyo kuna watu wanakula rushwa kila siku wakijua ni posho na kuna wengine wanakataa posho wakidhani ni rushwa.